# FURSA ZA UWEKEZAJI NA UTOAJI WA HUDUMA KATIKA KAMPASI MPYA YA UDSM KAGERA

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinapenda kuufahamisha umma, taasisi za umma na binafsi, makampuni, wafanyabiashara na watoa huduma kuhusu fursa za uwekezaji na uendeshaji wa biashara zinazopatikana katika Kampasi mpya ya UDSM Kagera, eneo la Kwauso katika vijiji vya Itahwa/Kangabusharo, Wilaya ya Bukoba, Mkoa wa Kagera.

Kampasi inatarajiwa kuanza shughuli za kitaaluma katika mwaka wa masomo 2026/2027 ikiwa na takribani wanafunzi 200 katika hatua ya awali, pamoja na watumishi, wageni na watumiaji wengine wa Kampasi. Kadiri shughuli za Kampasi zitakavyopanuka, idadi ya watumiaji na mahitaji ya huduma mbalimbali yanatarajiwa kuongezeka.

Katika maandalizi ya kuanza kwa shughuli za Kampasi na kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu kwa jamii ya Chuo, UDSM inawaalika watu binafsi, makampuni na wafanyabiashara wenye sifa, uwezo na nia ya kuendesha biashara katika Kampasi kuwasilisha maombi yao. Kuna makundi mawili ya uwekezaji: kundi la kwanza ni fursa ambazo zinaombwa kwa kujaza fomu maalum  na kundi la pili ni fursa zinazoombwa kupitia Mfumo wa Taifa wa Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki (NeST)

Makundi maalum (vijana, wanawake na wenye ulemavu) wanahamasishwa kushiriki katika fursa hizi.

## Sehemu ya I: Fursa Zinazoombwa kwa Kujaza Fomu Maalum

Fursa zifuatazo zinaombwa kwa njia ya waombaji kujaza fomu maalum:

| Na. | Huduma | Idadi ya Nafasi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 3 | Mini Supermarket | 1 | Bidhaa za matumizi ya kila siku. |
| 4 | Pharmacy/Duka la Dawa | 1 | Huduma za dawa baridi za binadamu, kwa kuzingatia masharti ya mamlaka husika. |
| 5 | Barber Shop (Saluni ya Kiume) | 1 | Huduma za saluni ya kiume. |
| 6 | Ladies Beauty,  Cosmetics & Salon | 1 | Saluni ya wanawake, vipodozi na huduma za urembo. |
| 7 | Steshenari | 1 | Huduma za steshenari na mahitaji yanayohusiana. |

### Fomu ya Maombi na Ada ya Fomu

Waombaji wanatakiwa kujaza Fomu ya Maombi ya Kupangisha Maeneo ya Biashara. Fomu inapatikana kupitia kiungo na QR Code iliyowekwa kwenye tangazo hili. Ada ya fomu ni **TZS 10,000/=** na italipwa kopitia Ankara ya Malipo (Control Number) itakayotolewa na Chuo kupitia Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji mwenye namba 0653 488 881.  Risiti/uthibitisho wa malipo lazima uambatishwe kwenye kifurushi cha maombi (application package).

https://udsm.ac.tz/sites/default/files/2026-08/FOMU_YA%20_AOMBI_KWA_MAENEO_YA_UWEKEZAJI_UDSM.pdf

### Namna ya Kuwasilisha Maombi

Kifurushi kamili cha maombi kijumuishe Fomu ya Maombi iliyojazwa kikamilifu, nyaraka zote zinazotakiwa na risiti/uthibitisho wa malipo ya **TZS 10,000/=**. Nyaraka zote ziskaniwe na kuunganishwa katika faili moja la PDF na kutumwa kwa barua pepe **dpdi@udsm.ac.tz** na nakala (CC) kwa **rugazia.godebertha@udsm.ac.tz**. Waombaji wanashauriwa kusoma kwa makini masharti yaliyoainishwa katika Fomu ya Maombi kabla ya kuwasilisha maombi. Waombaji wanapaswa kuhakikisha kuwa maombi yao yamekamilika kabla ya kuwasilishwa.

### Mawasiliano kwa Waombaji Kupitia Fomu Maalum

Mkurugenzi
Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35091, Dar es Salaam
Tovuti: www.udsm.ac.tz

### Mwisho wa Kuwasilisha Maombi

Tarehe na muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi tarehe **22 Oktoba 2026 saa tisa kamili alasiri (9:00 Alasiri)**. Maombi yatakayowasilishwa baada ya muda uliowekwa hayata pokelewa. Chuo kitafanya tathmini ya maombi yaliyopokelewa kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa na kutoa majibu kwa waombaji wote walioshinda na walioshindwa.

## Sehemu ya II: Fursa Zinazoombwa Kupitia Mfumo wa NeST

Fursa zifuatazo zinaombwa kupitia mfumo wa NeST:

| Na. | Aina ya huduma | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Huduma ya chakula | Huduma za chakula kwa wanafunzi na wafanyakazi katika Kampasi ya Kagera-Wilaya ya Bukoba. |
| 2 | Huduma ya ulinzi | Huduma za ulinzi wa maeneo ya Chuo yaliyopo Kwauso- katika vijiji vya Itahwa/Kangabusharo, Wilaya ya Bukoba. |
| 3 | Huduma ya usafi na usimamizi wa mazingira | Huduma za usafi na usimamizi wa mazingira katika maeneo ya Chuo yaliyopo Kwauso katika vijiji vya Itahwa/Kangabusharo, Wilaya ya Bukoba. |

Kwa kundi hili la fursa, zabuni rasmi na nyaraka zake zimetangazwa kupitia Mfumo wa NeST, https://www.nest.go.tz. na waombaji watawasilisha zabuni kwa kufuata maelekezo ya mfumo huo.Vigezo, masharti na tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi vinapatikana kwenye mfumo. Ni muhimu kwa waombaji kujisajili kwenye mfumo ili kuweza kuwasilisha maombi yao.

### Mawasiliano kwa Waombaji Kupitia Mfumo wa NeST

Meneja
Kitengo cha Ununuzi
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35091, Dar es Salaam
Barua pepe:
Tovuti: www.udsm.ac.tz.

### Kutembelea Maeneo ya Biashara (Site Visit)

Waombaji kupitia fomu maalum na waombaji kupitia mfumo wa NeST wanahimizwa kutembelea maeneo yanayotangazwa kabla ya kuwasilisha maombi ili kujionea mazingira na nafasi husika. Ziara ya maeneo itafanyika **tarehe 19/10/2026-kagera na 20/10/2026-Katelelo saa nne kamili asubuhi (10:00 a.m.)**. Gharama za kuhudhuria kutembelea maeneo zitagharimiwa na waombaji wenyewe.

### Muhimu Kwa Waombaji Wote

Waombaji wote wanafahamishwa kuwa, isipokuwa kwa huduma za usafi na ulinzi, utoaji wa huduma katika Kampasi hizi utaanza tu baada ya Uongozi wa Chuo kutoa idhini rasmi ya Kampasi kuanza shughuli za kitaaluma. Tarehe rasmi ya kuanza kutoa huduma itawasilishwa kwa watoa huduma watakaofanikiwa baada ya idhini hiyo kutolewa.